

Vodacom Tanzania Public Limited Company

(Imesajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)

(Namba ya usajili 38501)

(ISIN: TZ1996102715 Ticker code: VODA)

('Vodacom Tanzania' au 'Kampuni')

Taarifa ya kuteuliwa Mjumbe wa Bodi

Bodi ya Wakurugenzi ya Vodacom Tanzania PLC inapenda kuwafahamisha kuwa imemteua Bw. Dejan Kastelic kuwa Mkurugenzi asiye mtendaji kujaza nafasi iliyoachwa wazi na Bw. Andries Delpport aliyejuzulu tarehe 18 Mei 2020. Uteuzi wa Bw. Kastelic umeanza rasmi tarehe 17 Agosti 2020.

Bw. Kastelic aliteuliwa kuwa Afisa Mkuu wa Teknolojia wa Vodacom Group, Afrika Kusini mwezi Agosti 2020. Kabla ya kujiunga na Vodacom, alikuwa Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari katika kampuni ya PT Indosat Ooredoo TBK, sehemu ya kampuni ya Kundi la makampuni ya Ooredoo huko Qatar. Aidha, aliwahi kuwa Mkurugenzi wa kampuni ya Indosat, Singapore na ni Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi wa Posta Slovenije d.o.o. Bw. Kastelic alianza kazi katika kampuni ya simu Amis Ltd hadi kufikia nafasi ya Afisa Mkuu wa Teknolojia. Mwaka 2009 alihamia kampuni ya IBM Ulaya Mashariki na Kati kama Meneja Usimamizi wa Rasilimali. Mwaka 2012 alijiunga na kampuni ya Telekom Austria akiwa kama Mkurugenzi Mtendaji na Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari na baadaye akawa Mkurugenzi wa Kundi na Afisa Mkuu wa Teknolojia na Habari akisimamia kampuni za simu - Vip mobile, Serbia na Si.Mobil Slovenia. Mwaka 2015, alihamishiwa kampuni ya Mobilnet Bulgaria hadi alipoteuliwa kwenye nafasi aliyoshikilia mwanzo katika kampuni ya Indosat.

Bw. Kastelic ana Shahada ya Sayansi katika Uhandisi Umeme kutoka Chuo kikuu cha Maribo kilichopo Slovenia. Amejiunga katika programu ya Usimamizi wa Biashara huko IEDC Bled na pia alisoma Chuo Kikuu cha Harvard kilichoko Boston Marekani na INSEAD.

Bodi inachukua nafasi hii kumpongeza Bw. Kastelic katika uteuzi wake na inamtakia kila la kheri katika majukumu yake kama Mjumbe wa Bodi.

Kwa idhini ya Bodi.



Caroline Mduma

Katibu wa Kampuni

25 Agosti 2020

Uko Tayari?

